**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI**

**MKUTANO WA SITA**

**Kikao cha Pili – Tarehe 17 Februari, 2022**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara, na Utalii:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara, na Utalii ya mwaka 2021/2022.

**Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:**

Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Mwaka 2021/2022.

## II. MASWALI:

**Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:**

31. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

    Hivi karibuni kumekuwa na ongezeko kubwa la omba omba ndani ya Mkoa wa Mjini Magharibi ambao zipo taarifa kuwa wanatoka nje ya visiwa vya Zanzibar.

(a) Je, Serikali imelibaini tatizo hilo.

(b) Hatua gani zimechukuliwa kuwaondoa omba omba hao na kuwarudisha walipotoka.

**<u>Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:</u>**

2. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Zanzibar ni nchi yenye idadi kubwa zaidi ya Waislamu kuliko dini nyengine na pamoja na kuwa Serikali yetu haina dini, inaheshimu sana imani za wananchi wake. Katika kukuza uchumi wa nchi hii, Serikali yetu iliruhusu kuanzishwa kwa Benki ya Kiislamu, ili kuongeza mapato lakini pia kuheshimu imani za wananchi wake wa dini ya Kiislamu.

(a) Kwa nini Serikali haianzishi Bima ya Kiislamu kama ilivyoanzisha Benki ya Kiislamu.

(b) Je, kwa kiasi gani kutoanzishwa kwa Bima ya Kiislamu nchini kunaipotezea mapato Serikali yetu kama ilivyokuwa ikiyakosa kabla ya kuanzishwa kwa Benki ya Kiislamu.

**<u>Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:</u>**

67. MHESHIMIWA ABDALLA ABASS WADI (Jimbo la Nungwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Kumekuwa na malalamiko kwa vituo vya afya vya Nungwi, Tazari na Kidoti kwamba vituo hivi havina vifaa vya kupimia damu na wajawazito.

Kwa vile tayari vifaa hivi vimeshaombwa. Je, ni lini Wizara itachukua hatua ya kuvipatia vifaa hivyo vituo hivi.

121. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto:

Ugonjwa wa kisukari umekuwa ni changamoto katika visiwa vyetu vya Zanzibar ambapo hupelekea ulemavu na vifo na wengi wa wagonjwa hawa huelekea katika tiba za asili kutokana na kukosa imani kutoka kwa madaktari. Hali hii imesababishwa na

kuchelewa kupona kwa wagonjwa wengi wa namna hii. Pia Wizara haina mpango wa kuwaelimisha wananchi juu ya ugonjwa wa kiharusi.

(a) Kwa namna gani Wizara imejipanga kutambua aina za ugonjwa wa kiharusi na kuwapatia wananchi wetu tiba sahihi.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuwezesha upatikanaji wa dawa aina ya "mannitol" na kuwepo kwa wataalamu wa kutambua aina ya ugonjwa wa kiharusi katika hospitali zetu.

(c) Je, Wizara inajipanga vipi kuhakikisha inawapa ushauri na matumaini wagonjwa wengi wanaoelekea kwa waganga wa kienyeji kupata tiba kutokana na kukosa imani na tiba za hospitali.

**<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>**

10. MHESHIMIWA FATMA RAMADHAN MOHAMMED (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Naipongeza Serikali kwa juhudi za kutenga viwanja kwa ajili ya michezo lakini baadhi ya viwanja huvamiwa na wanaojifundishia magari.

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa wale wanaotumia viwanja hivi kwa ajili ya kufundishia magari.

**<u>Wizara ya Maji, Nishati na Madini:</u>**

61. MHESHIMIWA SHAIB HASSAN KADUARA (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Naipongeza Serikali yetu kwa kujitahidi kutekeleza ahadi zake inazozitoa kwa wananchi. Miongoni mwa ahadi alizozitoa Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA) kwa niaba ya Serikali, ni kutuahidi sisi wananchi wa Chanjaani kupata maji safi na salama ndani ya miezi mitatu kupitia kisima chetu cha Chanjaani, ingawaje sasa tuna miezi miwili imeshapita bila ya dalili yoyote ya kutekelezwa kwa ahadi hiyo.

(a) Je, Wizara yako inaikumbuka ahadi ya Mkurugenzi Mkuu wa ZAWA kwa wananchi wa Chanjaani.

(b) Je, tutegemee nini sisi wananchi wa Chanjaani juu ya kutekelezwa kwa ahadi hiyo.

**<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>**

46. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi.

Kumekuwa na malalamiko ya wafanyabishara wa Zanzibar kwamba mizigo yao wanayoagiza kutoka nje inachelewa sana kufika Zanzibar. Aidha, gharama za usafirishaji zimepanda toka US $ 2500 hadi US $ 7000 kwa kontena la futi 20 kutokana na baadhi ya makampuni ya meli kugoma kushusha mizigo katika bandari ya Zanzibar hivyo bidhaa zao kushushwa katika bandari za nchi nyengine ikiwemo Mombasa na Dar es Salaam, hivyo kuleta usumbufu na gharama kubwa.

(a) Kwa kuwa kilio hicho kina uzito mkubwa Je, Serikali inatoa msimamo gani.

(b) Ni makontena mangapi yaliyoshushwa katika bandari ya Mombasa ambayo yalitakiwa kuja Zanzibar kwa kipindi cha Januari – Julai, 2021.

55. MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (Jimbo la Shaurimoyo) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa muda mrefu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kuanzia awamu ya tano hadi awamu ya nane kumekuwa kukizungumziwa ujenzi wa bandari ya Mpigaduri na wananchi wamekuwa na matumaini makubwa na kauli ya Serikali zao hizi zote. Lakini tatizo awamu hizo zote humaliza bila ya bandari hiyo kujengwa na kwenye bajeti iliyopita pia bandari hii imetajwa katika vipaumbele vya Serikali hii ya awamu ya nane.

(a) Je, Wizara inatuambiaje katika suala hili la ujenzi wa bandari hii, lipo au halipo.

(b) Kama lipo Je, ujenzi huu unategemewa lini kuanza na kukamilika kwake.

(c) Je, Kampuni gani ambayo imepewa kazi hiyo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

89. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Taaluma ya ujasiriamali kwa sasa imekuwa ni jambo lisiloepukika katika kuwawezesha wananchi kujitegemea kiuchumi na kuondoa ukakasi wa ukosefu wa ajira.

Je, Wizara yako haioni kwamba ipo haja ya kuliingiza somo hili kwenye mtaala wa kufundishia, licha ya kwamba somo hili limekuwa likifundishwa katika vyuo na taasisi mbali mbali.

95. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Walimu Wakuu wanapoteuliwa hupatiwa barua za uteuzi kwa ajili ya taarifa rasmi.

(a) Je, kwa nini inachukua muda kupatiwa posho lao.

(b) Je, wanapopatiwa posho hilo la dhamana hupatiwa pia malimbikizo yao.

(c) Je, walimu wakuu ambao wanakaimu hawapatiwi posho lolote.

**Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:**

139. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali na Jumuiya za Kimataifa zinazojali afya za watu wake zimekuwa zikihimiza na kutilia mkazo shughuli za kilimo hai kwa lengo la kuwa na vyakula salama kwa matumizi ya binadamu. Hata hivyo, Serikali yetu haijajidhatiti katika kuelekea katika kilimo bila ya kemikali sambamba na uwepo wa vyakula salama.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi na mpango gani wa muda mrefu katika kutilia mkazo shughuli za kilimo hai.

(b) Je, Serikali inawasaidiaje wakulima wa jimbo la Pandani ambao, pamoja na shughuli nyengine, wanazalisha mbolea na madawa ya asili kwa ajili ya kilimo hai.

(c) Je, ni miradi gani ya kilimo hai ya Serikali inayowanufaisha wananchi wa jimbo la Pandani na kwa kiwango gani.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

107. MHESHIMIWA MTUMWA PEYA YUSSUF (Jimbo la Bumbwini) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Azma ya kuwa na Uchumi wa Buluu katika nchi yetu ni kuwakomboa wananchi wa Zanzibar.

(a) Je, vijana wetu tumewaandaaje kuwapatia elimu inayoendana na dhana mzima ya Uchumi wa Buluu.

(b) Kwa nini kusiwe na mitaala ya elimu kwa skuli za Sekondari yenye dhana hiyo.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

96. MHESHIMIWA JUMA ALI KHATIB (Uteuzi wa Rais) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Mnamo mwaka 2001 vijana 15 katika kijiji cha Sazani kilichopo Mjimbini katika Wilaya ya Mkoani Kisiwani Pemba, waliunganisha nguvu zao na kuunda kikundi kinachoitwa 'nguvu' ambapo waliamua kujiajiri wenyewe kwa kuanzisha kiwanda cha kutengeneza mafuta ya karafuu yatokanayo na majani makavu ya mikarafuu. Kwa kipindi kirefu kikundi hiki kilikuwa kikiliuzia Shirika la ZSTC mafuta hayo ya karafuu kwa bei ya Tsh. 500,000 kwa dumu moja lenye ujazo wa lita 20, na kwa hivi sasa Shirika hilo la ZSTC linanunua mafuta hayo kwa bei ya Tsh. 250,000 kwa dumu moja.

Kwa kuwa kuna taarifa kuwa bei ya mafuta hayo hivi sasa imepanda katika soko la dunia, na kwa kuwa kikundi hiki kilikuwa na makubaliano na uongozi wa ZSTC wa kipindi hicho kuwa bei ya mafuta hayo ikipanda katika soko la dunia na Shirika litapandisha bei ya kununulia mafuta hayo.

(a) Je, ni kwa nini Shirika la ZSTC halijapandisha bei ya kununulia mafuta hayo kutoka kwa wazalishaji hao wakati bei ya bidhaa hiyo imepanda kwa hivi sasa.

(b) Je, ni lini Shirika la ZSTC litakaa pamoja na vijana hao ili kufikiria juu ya kununua mafuta hayo kwa bei nzuri zaidi inayoendana na soko la hivi sasa.

(c) Je, Shirika la ZSTC limejipanga vipi kuwaendeleza kimafunzo vijana hawa ambao wameunganisha nguvu zao kwa ajili ya kuongezea thamani mkarafuu kwa kuzalisha bidhaa inayotokana na majani tu ya mkarafuu.

**<u>Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:</u>**

33. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwa kuwa migogoro ya ardhi inaongezeka siku hadi siku pamoja na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali.

Je, Serikali ina mpango mkakati gani ambao ni madhubuti na unaotekelezeka wa kuweka matumizi bora ya ardhi Zanzibar na kutatua migogoro ya ardhi kwa wananchi.

## III. HOJA ZA KAMATI:

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa</u>:**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya mwaka 2021/2022.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara, na Utalii:</u>**

Hotuba ya kuwasilisha Ripoti ya Kamati ya Kilimo, Biashara, na Utalii ya mwaka 2021/2022.

<u>Mwenyekiti wa  Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:</u>

Ripoti ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati ya Mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,**
**17 Februari, 2022.**

**(Raya Issa Msellem)**
**<u>KATIBU WA BARAZA</u>.**